
# Usafirishaji shirikishi utakavyoendesha Dira 2050

Habarileo Afrika Mashariki Septemba 9, 2025 Pg 9



Ndege, reli ya kisasa na bandari ni miongoni mwa miundombinu inayoimarisha usafiri na usafirishaji Tanzania.



Na Mwandishi Wetu

JULAI mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (maarufu kama Dira 2050) inayolenga kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha juu cha kati.

Aidha, inalenga kuifanya Tanzania kuwa shirikishi na yenye ustahimilivu katika kipindi cha miaka 25 ijayo.

Mpango huu wa kijasiri, unaoendeleza malengo ya Dira ya 2025 iliyozinduliwa mwaka 2000, umetambua 'vichocheo vitano' muhimu vitakavyoiwezesha Tanzania kuwa na uchumi wa thamani ya Dola za Marekani trilioni moja ifikapo mwaka 2050.

Dira hiyo itatekelezwa kupitia uwekezaji katika viwanda, kilimo, huduma, madini, utalii na ujenzi, ikiongozwa na ukuaji wa sekta binafsi, uboreshaji wa mazingira ya biashara na ushirikishwaji wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Vichocheo hivyo vilivyotambuliwa ni usafirishaji shirikishi, sayansi na teknolojia, nishati, utafiti na maendeleo pamoja na mabadiliko ya kidijiti.

Lengo kuu ni kuongeza tija, ubunifu na ushindani katika sekta zote za uchumi.

Makala hii inalenga kufafanua zaidi kuhusu usafirishaji shirikishi na umuhimu wake kama mhimili wa uchumi.

Usafirishaji shirikishi unahusu uratibu wa kifasaha wa bidhaa, watu, huduma na taarifa katika mnyororo mzima wa usambazaji kutoka uzalishaji hadi usambazaji kwa kutumia miundombinu bora na mifumo ya kidijiti.

Katika miaka ya karibuni, Tanzania imepiga hatua kubwa kuboresha uwezo wa usafirishaji kupitia maendeleo ya kimkakati ya miundombinu, mageuzi ya kimuundo na matumizi ya teknolojia, ikitumia nafasi yake ya kijiografia kama lango kuu la Afrika Mashariki na Kusini.

Maendeleo muhimu ni pamoja na uwekezaji mkubwa katika bandari, barabara, Reli ya Kisasa (SGR) pamoja na upanuzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege.

Miradi hiyo imeimarisha miundombinu ya ndani na kuongeza uhusiano wa mipakani, hivyo kuwezesha biashara ya kikanda na ushirikiano wa kiuchumi.

Inaendelea Uk. 10

Habari Leo Afrika Mashariki Septemba 9, 2025 Pg13



# Usafirishaji Shirikishi Utakavyoendesha Dira 2050

Inatoka Uk. 9



Treni ya reli ya kisasa (SGR)

Pia, Dira ya 2050 inasisitiza kwamba kuanzishwa kwa Vituo vya Pamoja vya Mipakani (OSBPs) kumerahisisha biashara ya kuvuka mipaka huku matumizi ya teknolojia za kidijiti yakiboresha taratibu za nyaraka, usimamizi wa ghala, ufuatiliaji wa shehena na ufanisi wa jumla wa mnyororo wa usambazaji.

Maendeleo haya yanaifanya Tanzania kuwa kitovu muhimu cha usafirishaji na biashara katika eneo hili na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi endelevu.

Hata hivyo, bado zipo changamoto hasa gharama kubwa za uendeshaji na ucheleweshaji.

Mpango unaonesha kuwa, kwa sasa usafirishaji unachangia kati ya asilimia 35 hadi 45 ya gharama za jumla za uagizaji bidhaa (pamoja na bima na usafirishaji), kiwango ambacho kimeifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi ghali zaidi duniani.

Gharama hizo zinachangiwa na muda mrefu wa kusubiri na kushusha mizigo unaosababishwa na mitandao ya usafirishaji isiyokamilika na yenye mapungufu.

Malengo ya Dira ya 2050 ni kuifanya Tanzania kuwa lango bora zaidi kwa Afrika Mashariki na Kusini, ikitumia nafasi yake ya kijiografia na kunufaika na uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya biashara, hivyo kuwezesha biashara isiyo na vikwazo mipakani.

Aidha, mpango huu unalenga kuifanya Tanzania kuwa njia kuu ya biashara ya usafirishaji na kitovu cha biashara na usafirishaji kwa Afrika Mashariki na Kati.

Mpango huu unaazimia kuwa na mtandao wa usafirishaji shirikishi wenye mfumo wa usafiri wa aina mbalimbali na miundombinu ya kisasa inayounganisha korido za kiuchumi ili kuwezesha biashara ya ndani na ya kimataifa kwa ufanisi.

Pia, Dira inalenga kuwa na watoa huduma bora wa usafirishaji wenye ubora wa kimataifa na gharama shindani, kupitia teknolojia za kisasa za kidijiti ili kuongeza ufanisi na mtiririko rahisi wa taarifa katika mnyororo wa thamani.

Ili kufanikisha Dira ya 2050, lazima kuwe na mazingira yenye uwazi na ufanisi yatakayopunguza urasimu, kurahisisha taratibu za forodha, kutumia teknolojia za usafirishaji na kuhakikisha uzingatiaji wa viwango vya kimataifa.

Mwisho kabisa, mtandao wa usafirishaji shirikishi unapaswa kuwa jumuishi na unaopatikana kwa wote, ukiwa na miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu ili kuhakikisha ushiriki sawa na urahisi wa kusafiri ndani na nje ya nchi.

Kwa kuzingatia malengo ya Dira ya 2050 kupitia vichocheo vitano vya uchumi, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia imechukua hatua mbalimbali kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafirishaji katika kanda.

Uwekezaji mkubwa umefanyika kuboresha bandari za Bahari ya Hindi kupitia miradi kama Dar es Salaam Maritime Gateway Project (DMGP) inayolenga kuongeza ufanisi na uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam, ikiwemo kuchimba kina cha gati, kupanua njia ya kuingilia na kujenga gati jipya la mizigo mchanganyiko.

Mradi huu ambao pia unahusisha kuimarisha taasisi, unakusudia kuibadilisha bandari hiyo kuwa ya viwango vya kimataifa, kuongeza uwezo wa kushughulikia mizigo na kuchochea maendeleo ya kiuchumi ya Tanzania na nchi jirani zisizo na pwani.

Aidha, upanuzi wa Bandari ya Tanga kwa gharama ya zaidi ya Sh bilioni 400 umeboresha miundombinu yake, ikiwemo uchimbaji wa ghuba na ujenzi wa gati jipya.

Kwa upande mwingine, uboreshaji wa Bandari ya Mtwara unalenga kuongeza uwezo wake na kuifanya kitovu muhimu cha usafirishaji kwa Kusini mwa Tanzania na nchi jirani kama Malawi, Zambia na Msumbiji.

Mbali na bandari za pwani, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) inajenga bandari mpya katika maziwa ya ndani kama vile Bandari ya Kalema katika Ziwa Tanganyika pamoja na kuboresha bandari nyingine katika Ziwa Victoria na Ziwa Nyasa.

Vilevile, mipango ipo ya kujenga bandari kubwa ya Bagamoyo itakayosaidia kupunguza msongamano wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam.

Hivi karibuni, Tanzania imeendelea kujiimarisha kama kitovu cha usafirishaji na biashara kikanda kwa kuzindua Kituo cha Kimataifa cha Usafirishaji cha Kwala kilichopo mkoani Pwani. Kituo hicho kinalenga kurahisisha uondoshaji mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam.

Kituo hiki kilichozinduliwa Julai 31, mwaka huu kipo umbali wa kilometa 90 kutoka Bandari ya Dar es Salaam na kilometa 15 kutoka barabara kuu ya Dar es Salaam-Morogoro na kina eneo la jumla la ekari 502, takribani mara tano ya ukubwa wa bandari yenyewe.

Kituo hicho cha Kwala kinatarajiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa muda na gharama za usafirishaji kwa wafanyabiashara wa ndani na nje wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam kuagiza au kusafirisha mizigo.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Rais Samia anasema kituo hicho kitarahisisha huduma za usafirishaji na kukuza fursa za biashara kwa Watanzania na wananchi wa nchi jirani.

Anabainisha kuwa kituo hicho kitaifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafirishaji na biashara katika Afrika Mashariki na Kati sambamba na utekelezaji wa Eneo Huru la Biashara barani Afrika (AfCFTA).

"Kituo cha Kwala kitasaidia usafirishaji wa mizigo kwenda na kutoka DRC, Zambia, Burundi, Rwanda, Malawi na Uganda," anasema.

Anaongeza: "Kwa kufanya hivyo kutaongeza ushindani wa Bandari ya Dar es Salaam katika eneo hili."

Kwa upande wa miundombinu ya reli, Rais Samia anasema mipango inaendelea kuunganisha Kituo cha Kwala na Bandari ya Tanga (takribani kilometa 256) pamoja na Bandari ya Bagamoyo (takribani kilometa 60).

"Mpango upo wa kujenga bandari kubwa ya kina kirefu Bagamoyo itakayoweza kuhudumia meli kubwa zenye uwezo wa kubeba hadi makontena 6,000 kwa safari moja. Bandari hiyo pia itaunganishwa na Kwala," anaeleza.

Kwa kuunganisha huduma za reli na baharini, muda wa usafirishaji mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam hadi Kampala, Uganda, unatarajiwa kupunguzwa kutoka siku 15 hadi16 hadi siku tano hadi sita pekee.

Pia, Rais Samia anasema kiwango cha mizigo kinachoshughulikiwa katika Bandari ya Dar es Salaam kimeongezeka kutoka tani milioni 23.69 mwaka 2023 hadi tani milioni 27.76 mwaka 2024.

Aidha, idadi ya meli zinazotia nanga bandarini humo imeongezeka kutoka 1,860 hadi 1,990 katika kipindi hicho.

Kimsingi wadau mbalimbali wanasema uboreshaji wa bandari, viwanja vya ndege, barabara na reli utasaidia si tu kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafirishaji, bali pia kuchochea kufanikisha Dira ya 2050.

CamScanner



Manyara Regional Traffic Police Commander Michael Mwakasungura pictured in Babati town at the weekend sensitising bus passengers on the importance of knowing their rights and obligations. Photo: Guardian Correspondent

CamScanner

Mwananchi Septemba 9/2025
Pg1




# Kunradhi UDART

Mwananchi Septemba 9,2025 Pg 6

## KUNRADHI UDART

Katika toleo letu la Gazeti la Mwananchi la Septemba 2, 2025 tulichapisha habari yenye kichwa cha habari: **MWENDOKASI MBAGALA, WAKAZI DAR SASA WAKERWA AHADI HEWA ZA UDART.**

Habari hiyo ilikuwa ikihusu kusogezwa mbele kuanza kwa utoaji wa huduma ya usafiri kwa mabasi ya mwendokasi kuanzia Mbagala hadi Gerezani na taarifa hiyo ilitolewa na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (Dart).

Hata hivyo, kwenye kichwa cha habari cha taarifa hiyo badala ya kuandika Dart tuliandika Udart kwa makosa.

Kwa sababu hiyo, tunaomba radhi uongozi wa Udart na wasomaji wetu kwa usumbufu uliosababishwa na dosari hiyo.

***Mhariri Mtendaji- Mwananchi***

CS CamScanner